

**Abstract:**

Tasnifu hii imehakiki na kutathmini mwingilianomatini katika riwaya mbili za waandishi tofauti: Rosa Mistika (Kezilahabi) na Tata za Asumini (Ahmed). Tasnifu yenyewe ina sura tano. Katika sura ya kwanza tumeshughulikia tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete, sababu za kuchagua somo, msingi wa nadharia, up eo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mwingilianomatini na aidha njia zilizotumika katika utafiti huu. Katika sura ya pili tumefafanua istilahi au dhana ambazo hususan hutumika katika kuhakikia na kutathminia umwingilianomatini. Dhana hizi tumeziita 'vipengele katika mwanda wa kimwingilianomatini.' Mathalani: wahusika, maudhui, mandhari na aidha msuko. Sura ya tatu imejadili mwingilianomatini wa uhusika katika riwaya hizi mbili kwa kuangazia baadhi ya wahusika na sifa zao. Aidha, sura ya nne imeshughulikia mwingilianomatini wa kimaudhui. Hapa maudhui ya ujaala, dhuluma dhidi ya mwanamke, kukata tamaa na aidha malezi yamehakikiwa kwa mujibu wa nadharia ya umwingilianomatini. Utafiti wetu umehitimishwa katika sura ya tano. Aidha tumetoa mapendekezo kuhusu sehemu ambazo zinaweza kufanyiwa tahakiki siku zijazo.